قيام رمضان

Qiyaam Ramadhwaan

[Kisimamo cha Ramadhaan]

Mwandishi:

Imaam Muhammad Naaswir-ud-Diyn al-Albaaniy

Tarjama:

Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush

Utangulizi wa chapa ya pili....3
Fadhila za kusimama nyusiku za Ramadhaan....4
Laylat-ul-Qadr na mpaka wake....4
Shari´ah ya kuswali mkusanyiko....5
Sababu ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kutoendelea kuswali mkusanyiko....6
Shari´ah ya wanawake kuswali mkusanyiko....6
Idadi ya Rak´ah katika swalah....7
Kisomo katika swalah....8
Wakati wa swalah....9
Namna za kuswali swalah ya usiku....11
Kisomo katika Witr ambayo ni Rak´ah tatu....12
Du´aa za Qunuut na mahala pake....13
Kipi kinachosemwa mwishoni mwa Witr?....14
Rak´ah mbili zinazofuata....14
I´tikaaf na kuwekwa kwake katika Shari´ah....15
Sharti zake....16
Ni yepi yanayojuzu wakati wa I´tikaaf?....17
Inafaa kwa mwanamke kufanya I´tikaaf na kumtembelea mume wake msikitini....18

[Kwa jina la Allaah, Mwingi wa huruma, Mwenye kuhurumia]

Utangulizi wa chapa ya pili

Himdi zote zinamstahikia Allaah na swalah na salaam zimwendee Mtume wa Allaah, kizazi chaeke, Maswahabah wake na wale wote watakaofuata Sunnah na mwongozo wake.

Amma ba´d:

Hii ni chapa ya pili ya kitabu changu "Qiyaamah Ramadhwaan" ninachomuwakilishia muheshimiwa msomaji kwa mnasaba wa kukaribia mwezi wa Ramadhaan uliyobarikiwa 1406. Haya ni baada ya kuuzikana chapa ya kwanza na kukaulizwa sana juu yake. Ndipo ikabidi nikipitie kwa mara nyingine, kukichakachua na kuongeza idadi zaidi ya mapokezi ya Hadiyth na faida na masomo mepya ambayo - Allaah akitaka - yatawafurahisha wasomaji. Miongoni mwa mambo muhimu atayoyaona msomaji ni suala la I´tikaaf.

Ninamuomba Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) anijaalie yale ya sawa yanizunguke, anisamehe makosa yangu, ailinde kalamu yangu nayo na vilevile aijaalie iwe imefanywa kwa ajili ya Uso Wake mtukufu - kwani hakika Yeye ni Mwingi wa kusamehe, mkarimu.

´Ammaan
Tarehe 07 Sha´baan 1406
Muhammad Naaswir-ud-Diyn al-Albaaniy

Fadhila za kusimama nyusiku za Ramadhaan

[1] Kumekuja Hadiyth mbili juu ya jambo hili.

Ya kwanza: Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ´anh) amesema:

> "Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akipenda kusimama nyusiku za Ramadhaan pasi na kuwaamrisha. Halafu akawaambia:
>
> "Atakayesimama nyusiku za Ramadhaan pamoja na imamu kwa imani na matarajio, basi atasamehewa madhambi yake yaliyotangulia."

Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akafariki na hali bado ikaendelea kuwa hivyo[1]. Kisha hali ikaendelea kuwa hali kadhalika katika ukhaliyfah wa Abu Bakr (Radhiya Allaahu ´anh) na vivyo hivyo mwanzoni mwa ukhaliyfah wa ´Umar (Radhiya Allaahu ´anh)."[2]

Ya pili: ´Amr bin Murrah al-Juhaniy amesema:

> "Kuna mwanamume kutoka Qudhwaa´ah alikuja kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kusema: "Ee Mtume wa Allaah! Unaonaje lau nitashuhudia ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah na kwamba wewe ni Mtume wa Allaah, nikaswali vipindi vitano, nikafunga mwezi, nikasimama nyusiku za Ramadhaan na nikatoa zakaah?" Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akasema: "Atakayekufa katika hali hii, basi atakuwa ni katika wakweli na mashahidi.""[3]

Laylat-ul-Qadr na mpaka wake

[1] Bi maana Tarawiyh kutoswaliwa kwa mkusanyiko.

[2] Muslim na wengineo. Imetajwa katika "al-Irwaa´" (04/14/906) na "Swahiyh Abiy Daawuud" (1241) - namuomba Allaah anisahilishie kukikamilisha na kukichapisha. Na kuhusu taaliki ya ndugu Zuhayr kwenye kitabu changu "Swalaat-ul-´Iydayn", uk. 32: "Allaah amemrahisishia mwalimu wetu al-Albaaniy kuchapisha sehemu ya kwanza ya "Swahiyh Abiy Daawuud", ninaapa kwa Allaah sijui ameyatoa wapi. Sehemu ya kwanza iko kwangu na sijampa yeyote idhini ya kuikopi, kuichapisha wala kuisambaza. Hali kadhalika yale aliyoyataja mwaka 1403 katika chapa ya nne ya kitabu changu "at-Tawassul", uk. 22, na kwamba mujaladi wa tatu wa "Silsilah al-Ahaadiyth adh-Dhwa´iyfah" umeshatoka. Leo ni tarehe 1406 Rajab na bado mpaka sasa hakijatoka!

[3] Ibn Khuzaymah na Ibn Hibbaan katika "as-Swahiyh" zao na wengineo. Mlolongo wa wapokezi ni Swahiyh. Tazama taaliki yangu ya "Ibn Khuzaymah" (03/340/2262) na "Swahiyh at-Targhiyb" (01/419/993).

[2] Usiku bora ni usiku wa makadirio kujengea maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

> "Yule mwenye kusimama usiku wenye cheo kwa imani na kwa matarajio kisha akawafikishwa nao, atasamehewa madhambi yake yaliyotangulia."[4]

[3] Maoni yenye nguvu yanasema kuwa ni usiku wa tarehe ishirini na saba Ramadhaan. Hadiyth nyingi zinasema hivo. Moja wapo ni Hadiyth ya Zirr bin Hubaysh aliyesema:

> "Nimesikia Ubayy bin Ka´b akiambiwa: "´Abdullaah bin Mas´uud anasema kwamba yule mwenye kuswali mwaka mzima basi ataupata usiku wa makadirio." Ndipo Ubayy (Radhiya Allaahu ´anh) akasema: "Allaah amuwie radhi kwani hakupenda watu wabweteke. Ninaapa kwa yule ambaye hakuna mungu mwengine wa haki asiyekuwa Yeye ya kwamba ni katika Ramadhaan. Ninaapa kwa Allaah pia kuwa najua ni usiku gani! Usiku ambao Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ametuamrisha tuswali ni usiku wa tarehe ishirini na saba. Alama yake ni jua kuchomoza asubuhi leupe likiwa halichomi.""

Katika upokezi mwingine amemnasibishia hayo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)[5].

Shari´ah ya kuswali mkusanyiko

[4] Imewekwa Shari´ah kuswali kwa pamoja swalah za nyusiku katika kisimamo cha Ramadhaan. Bali ndilo jambo bora kuliko mtu kuswali peke yake kujengea ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) yeye mwenyewe alifanya hivo na akaonyesha fadhila zake. Abu Dharr (Radhiya Allaahu ´anh) amesema:

---

[4] al-Bukhaariy, Muslim na wengineo kutoka kwa Abu Hurayrah na Ahmad (05/318) kutoka kwa ´Ubaadah bin as-Swaamit. Nyongeza ni ya kwake na vilevile Muslim kutoka kwa Abu Hurayrah. Tanbihi! Katika chapa iliyotangulia mwishoni mwa Hadiyth nilitaja nyongeza nyingine yenye kusema: "... na yatayokuja huko mbele." Nilikuwa nimemtegemea al-Mundhiriy na al-´Asqalaaniy waliosema kuwa ni Swahiyh. Kisha Allaah (Ta´ala) akanisahilishia kupeleleza njia nyenginezo za Hadiyth na mapokezi kutoka kwa Abu Hurayrah na ´Ubaadah kwa njia ambayo sijawahi kuona imefanywa na yeyote. Nikapata kubainikiwa kuwa ni nyongeza hiyo ni *Shaadhdh* kutoka kwa Abu Hurayrah *Munkar* kutoka kwa ´Ubaadah. Yule aliyeifanya hii kuwa nzuri na ile nyingine kuwa Swahiyh, amefanya hivo kwa kudanganyika na udhahiri wa mlolongo wa wapokezi pasi na kufuatilia njia nyenginezo za mapokezi. Nimeiweka katika "Silsilah al-Ahaadiyth adh-Dhwa´iyfah" (5083). Sikutaja nyongeza hii katika Hadiyth ya Abu Hurayrah kwa sababu nimeitaja katika "Swahiyh at-Targhiyb wat-Tarhiyb" (982). Hata hivyo sikutaja Hadiyth ya ´Ubaadah pamoja nayo tofauti na asili yake "at-Targhiyb" - na Allaah (Ta´ala) ndiye Mwenye kuwafikisha.

[5] Muslim na wengineo. Imetajwa katika "Swahiyh Abiy Daawuud" (1247).

"Tulifunga Ramadhaan pamoja na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wala hakuswali chochote katika mwezi mpaka kulipobaki siku saba. Ndipo akaswali na sisi mpaka kulipoenda thuluthi ya usiku. Hata hivyo [ule usiku wa] sita hakuswali na sisi isipokuwa alifanya hivo katika [ule usiku] wa tano [usiku wa 25] mpaka kukaenda nusu ya usiku. Nikasema: "Ee Mtume wa Allaah! Ungetuliswalisha tu usiku mzima." Akasema: "Mtu akiswali pamoja na imamu mpaka atakapomaliza, basi anazingatiwa ni kama ameswali usiku [mzima]."

Ule [usiku] wa nne hakuswali, lakini ulipofika [ule usiku wa] tatu[6], akaikusanya familia yake, wake zake na watu na akatuswalisha mpaka tukachelea kupitwa na kufuzu." Nikasema: "Kufuzu ni kitu gani?" Akasema: "Ni daku. Halafu hakutuswalisha mwezi uliobaki."[7]

Sababu ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kutoendelea kuswali mkusanyiko

[5] Sababu iliyomfanya (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kutoendelea kuswali na wao mkusanyiko mwezi uliobaki, ilikuwa ni kuchelea swalah za nyusiku zisije kufaradhishwa kwao katika Ramadhaan. Hiki ni kitu wasingekiweza, kama ilivyotajwa katika Hadiyth ya ´Aaishah katika "as-Swahiyh" ya al-Bukhaariy na Muslim na vyenginevyo[8]. Wasiwasi huu uliondoka kwa kufa kwake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) baada ya Allaah kukamilisha Shari´ah na kwa ajili hiyo mtu alikuwa anaweza kurudi kuswali nyusiku za Ramadhaan kwa mkusanyiko. Hukumu ya asili ikawa imebaki, ambayo ni kuswali kwa mkusanyiko, na kwa ajili hiyo ndio maana ´Umar (Radhiya Allaahu ´anh) akaihuisha, kama ilivyotajwa katika "as-Swahiyh" ya al-Bukhaariy na vyenginevyo[9].

Shari´ah ya wanawake kuswali mkusanyiko

[6] Bi maana usiku wa tarehe ishirini na saba na ndio Laylat-ul-Qadr kujengea maoni yaliyo na nguvu kama tulivyotangulia kusema. Kwa ajili hiyo ndio maana Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliikusanya familia yake na wakeze katika usiku huo na hapo kuna dalili yenye kuonyesha kuwa imependekezwa kwa wanawake kuhudhuria usiku huo.

[7] Hadiyth ni Swahiyh. Wameipokea watunzi wa "as-Sunan" na wengineo. Kadhalika imetajwa katika "Swalaat-ut-Taraawiyh", uk. 16-17, "Swahiyh Abiy Daawuud" (1245) na "al-Irwaa´" (447).

[8] Tazama "at-Taraawiyh", uk. 12-14.

[9] Tazama takhriyj ya Hadiyth hii na maneno ya Ibn ´Abdil-Barr na wengineo juu yake katika marejeo yaliyotangulia, uk. 49-52.

[6] Imewekwa katika Shari´ah kwa wanawake kuhudhuria swalah hizi kujengea Hadiyth ya Abu Dharr iliyotangulia. Bali inafaa kuwateulia imamu ambaye atakuwa ni wa kwao peke yao mbali na yule imamu wa wanaume. Imethibiti kuwa ´Umar (Radhiya Allaahu ´anh) pindi alipowakusanya watu juu ya swalah za nyusiku, alimteua Ubayy bin Ka´b kuwa imamu wa wanaume na Sulaymaan bin Abiy Hathmah kuwa wa wanawake. ´Arfajah ath-Thaqafiy amesema:

"´Aliy bin Abiy Twaalib (Radhiya Allaahu ´anh) alikuwa akiwaamrisha watu kuswali mwezi wa Ramadhaan na akiwateulia wanaume imamu na wanawake imamu na mimi ndiye nilikuwa imamu wa wanawake."[10]

Naonelea kuwa kitendo hichi ni sahihi ikiwa msikiti ni mpana ili wamoja wasiwashawishe wengine.

Idadi ya Rak´ah katika swalah

[7] Idadi ya Rak´ah ni kumi na moja. Tunaona kuwa mtu asizidishe juu ya hizo. Badala yake mtu anatakiwa kumfuata Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Hakuzidisha juu ya hizo mpaka alipofariki. ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anhaa) aliulizwa kuhusu swalah yake katika Ramadhaan ambapo akasema:

> "Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa hazidishi, si katika Ramadhaan wala nyingine, juu ya Rak´ah kumi na moja. Alikuwa akiswali nne, usiulize juu ya uzuri wake na urefu wake. Kisha akiswali tena nne, usiulize juu ya uzuri wake na urefu wake. Halafu akiswali tatu."[11]

[8] Hata hivyo inafaa kwa mtu kupunguza idadi yake, hata kama mtu ataswali Rak´ah moja ya Witr peke yake. Dalili ni kitendo na maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kuhusu kitendo chake, ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anhaa) aliulizwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akiswali Rak´ah ngapi za Witr. Ndipo akajibu:

[10] Hiyo na ile iliyo kabla yake amezipokea al-Bayhaqiy (02/494). Ya kwanza ameipokea vilevile ´Abdur-Razzaaq katika "al-Muswannaf" (4/258/8722) na Ibn Naswr ameipokea katika "Qiyaam Ramadhwaan", uk. 93, na ameitumia kama hoja kwa yale tuliyoyataja punde tu katika ukurasa wa 95.

[11] Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim. Imetajwa katika "Swalaat-ut-Taraawiyh", uk. 20-21, na "Swahiyh Abiy Daawuud" (1212).

"Alikuwa akiswali Witr kwa nne[12] na tatu, sita na tatu, kumi na kumi na moja na hakuwa anaswali Witr chini ya saba wala zaidi ya kumi na tatu."[13]

Ama kuhusu maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), amesema:

"Witr ni yenye kudumu. Yule anayetaka aswali Witr kwa tano, anayetaka aswali Witr kwa tatu na anayetaka aswali Witr kwa moja."[14]

Kisomo katika swalah

[9] Ama kuhusu kisomo katika swalah ya usiku Ramadhaan na miezi mingine, Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakuweka kiwango maalum kwa njia ya kwamba mtu hatakiwi kuzidisha juu yake wala kupunguza. Kisomo chake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na urefu wake ulikuwa unatofautiana. Wakati fulani alikuwa akisoma katika kila Rak´ah "al-Muzzammil" na Suurah hii ina Aayah ishirini na wakati mwingine akisoma kiasi cha Aayah khamsini. Alikuwa akisema:

"Atakayeswali usiku kwa Aayah mia moja basi hatoandikwa katika waghafilikaji."

Katika Hadiyth nyingine:

"... kwa Aayah mia mbili ataandikiwa katika wema na wenye *IKhlaasw*."

Usiku mmoja pindi alipokuwa mgonjwa, alisoma (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) zile Suurah saba, nazo ni "al-Baqarah", "Aal ´Imraan", "an-Nisaa´", "al-Maaidah", al-An´aam", "al-A´raaf" na "at-Tawbah".

Katika kisa cha Hudhayfah bin al-Yamaan (Radhiya Allaahu ´anh) swalah yake nyuma ya Mtume (´alayhis-Swalaatu was-Salaam), alisoma (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika Rak´ah moja "al-Baqarah", "an-Nisaa´" na "Aal ´Imraan" taratibu[15].

[12] Katika hizo kunaingia Rak´ah mbili za Sunnah baada ya ´Ishaa na Rak´ah mbili fupi ambazo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akianza swalah ya usiku kwazo. Haya ni maoni ya Haafidhw. Tazama "Swalaat-ut-Taraawiyh", uk. 19-20.

[13] Ameipokea Abu Daawuud, Ahmad na wengineo. Hadiyth ina mlolongo wa wapokezi mzuri ambao unazingatiwa kuwa Swahiyh na al-´Iraaqiy. Imetajwa katika "Swalaat-ut-Taraawiyh", uk. 98-99, na "Swahiyh Abiy Daawuud" (1233).

[14] Ameipokea at-Twahaawiy, al-Haakim na wengineo. Hadiyth ina mlolongo wa wapokezi Swahiyh kama walivyosema maimamu wengi. Ina Hadiyth nyingine mfano wake ilio na nyongeza ambayo ni munkari , kama nilivyobainisha katika "Swalaat-ut-Taraawiyh", uk. 99-100

[15] Hadiyth zote hizi ni Swahiyh na zimetajwa katika "Swifat Swalaat-in-Nabiyy", uk. 117-122.

Imethibiti kwa mlolongo wa wapokezi ulio Swahiyh zaidi ya kwamba pindi ´Umar (Radhiya Allaahu ´anh) alipomwamrisha Ubayy bin Ka´b kuwaswalisha watu katika swalah Ramadhaan kwa Rak´ah kumi na moja, alikuwa Ubayy (Radhiya Allaahu ´anh) akisoma Aayah mia mbili mpaka wale waliosimama nyuma yake wakitegemea bakora kutokana na urefu wa kisomo. Walikuwa wakibaki katika hali hiyo mpaka mwanzo wa alfajiri[16].

Imesihi pia kutoka kwa ´Umar ya kwamba aliwakusanya wasomaji katika Ramadhaan na akawaamrisha wale wasomao Qur-aan haraka wasome Aayah thelathini, wale wa kati na kati Aayah ishirini na tano na wale wasomao taratibu Aayah ishirini[17].

Kujengea juu ya hili yule anayeswali peke yake anaweza kurefusha anavyotaka. Vivyo hivyo ikiwa amezungukwa na wale wanaokubaliana nae. Kila ambavyo ni ndefu ndivyo inavyokuwa bora zaidi. Lakini hata hivyo asipindukii mpaka akaswali usiku mzima, kitu ambacho kinatakiwa kufanywa mara chache. Badala yake mtu anatakiwa kumfuata Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliyesema:

> "Uongofu bora ni uongofu wa Muhammad."[18]

Ama mtu akiwaongoza wengine katika swalah, awarefushie kwa njia isiyowatia uzito wale waswaliji walio nyuma yake. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

> "Mmoja wenu atapowaswalisha watu, basi aikhafifishe swalah yake. Kwani hakika nyuma yake kuna ambao ni wadogo, wazee, wadhaifu, wagonjwa na wenye haja. Ama akiswali peke yake, basi airefushe swalah yake apendavyo."[19]

Wakati wa swalah

[10] Wakati wa swalah ya usiku unaanza baada ya swalah ya ´Ishaa mpaka swalah ya al-Fajr. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

[16] Ameipokea Maalik na wengineo. Tazama "Swalaat-ut-Taraawiyh", uk. 52.

[17] Tazama marejeo yaliyotangulia, uk. 71. Vilevile imepokelewa na ´Abdur-Razzaaq katika "al-Muswannaf" (4/621/7731) na al-Bayhaqiy (2/498).

[18] Hiki ni kipande cha Hadiyth iliyopokelewa na Muslim, an-Nasaa´iy na wengineo. Imetajwa katika "Ahkaam-ul-Janaa-iz", uk. 18, na "al-Irwaa´" (759-760).

[19] al-Bukhaariy na Muslim na nyongeza ni ya Muslim. Imetajwa katika "al-Irwaa´" (512) na "Swahiyh Abiy Daawuud" (759-760).

"Hakika Allaah amekuzidishieni swalah nayo ni Witr[20]. Iswalini kati ya swalah ya ´Ishaa na swalah ya Fajr."[21]

[11] Lililo bora ni kuswali sehemu ya mwisho ya usiku kwa yule atayeweza kufanya hivo. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Anayechelea kutoweza kuamka sehemu ya mwisho ya usiku, basi aswali Witr mwanzo wake. Yule anayetumai kuamka mwisho wake, basi aswali sehemu ya mwisho ya usiku, kwa kuwa kuswali sehemu ya mwisho ya usiku kunashuhudiwa na ndio bora."[22]

[12] Endapo mtu atakhiyarishwa kati ya kuswali na mkusanyiko mwanzoni mwa usiku na kuswali peke yake mwishoni mwa usiku, inahesabika kuswali na mkusanyiko ndio bora zaidi. Hili ni kwa sababu atalipwa kuwa ameswali usiku mzima, kama ilivyotangulia kwenye nambari nne kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kadhalika matendo ya Maswahabah yalikuwa juu ya hilo kama ilivyokuwa wakati wa ´Umar (Radhiya Allaahu ´anh). ´Abdur-Rahmaan bin ´Abd al-Qaariy amesema:

"Usiku mmoja nilitoka mimi pamoja na ´Umar bin al-Khattwaab kwenda msikitini na tukakuta watu wametawanyika; mwanamume anaswali peke yake na mwengine anaswali na mkusanyiko. Akasema: "Ninaapa kwa Allaah ya kwamba mimi naonelea kuwa lau mtu atawakusanya wote nyuma ya msomaji mmoja basi ingelikuwa bora." Halafu akalishikilia na akawakusanya nyuma ya Ubayy bin Ka´b. Kisha usiku mwengine nikatoka naye na tukakuta watu wanaswali nyuma ya msomaji wao. Ndipo ´Umar akasema: "Ni uzuri wa uzushi uliyoje huu. Ile [sehemu ya usiku] wanayolala ni bora kuliko ile [sehemu] wanayoswali ndani yake." - anamaanisha sehemu ya mwisho ya usiku, watu walikuwa wanaswali sehemu ya mwanzo wa usiku."[23]

Zayd bin Wahb amesema:

"´Abdullaah alikuwa akituswalisha Ramadhaan na akimaliza inapokuwa usiku."[24]

[20] Swalah ya usiku yote inaitwa "Witr" kwa kuwa idadi yake ni witiri.

[21] Hadiyth ni Swahiyh. Ameipokea Ahmad na wengineo kutoka kwa Abu Baswiyr. Imetajwa katika "as-Swahiyhah" (108) na "al-Irwaa´" (2/158).

[22] Muslim na wengineo. Imetajwa katika "as-Swahiyhah" (2610).

[23] al-Bukhaariy na wengineo. Imetajwa katika "at-Taraawiyh", uk. 48.

[24] ´Abdur-Razzaaq (7741) na wengineo na mlolongo wa wapokezi wake ni Swahiyh. Imaam Ahmad ameashiria upokezi huu na ulio kabla yake pindi alipoulizwa: "Je, mtu acheleweshe swalah mpaka sehemu ile ya mwisho ya usiku?" Akajibu: "Hapana. Mwenendo wa waislamu ni wenye kupendeza zaidi kwangu."

Namna za kuswali swalah ya usiku

[13] Niliandika kwa upambanuzi suala hili katika "Swalaat-ut-Taraawiyh", uk. 101-115, na kwa hivyo napendelea kulitaja hilo hapa kwa ufupi kama kumsahilishia na kumkumbusha msomaji:

Njia ya kwanza: Rak´ah kumi na tatu. Inafunguliwa kwa Rak´ah mbili fupi na kwa mujibu wa maoni yaliyo na nguvu ndio zile Rak´ah mbili za Sunnah baada ya ´Ishaa au Rak´ah mbili maalum ambazo inafunguliwa swalah ya usiku kwazo kama tulivyotangulia kusema. Halafu anaswali Rak´ah mbili ndefu kabisa. Kisha anaswali Rak´ah mbili fupi kuliko zilizotangulia. Kisha anaswali Rak´ah mbili fupi kuliko zile mbili zilizo kabla yake. Halafu anaswali Rak´ah mbili fupi kuliko zile mbili zilizo kabla yake. Kisha anaswali Rak´ah mbili fupi kuliko zile mbili zilizotangulia na kisha anaswali Witr kwa Rak´ah moja.

Njia ya pili: Rak´ah kumi na tatu. Kunaswaliwa Rak´ah nane na kutolewa Tasliym kila baada ya Rak´ah mbili. Halafu aswali Witr kwa Rak´ah tano na asikae na wala asitoe Tasliym isipokuwa katika ile ya tano.

Njia ya tatu: Rak´ah kumi na moja. Atoe Tasliym kila baada ya Rak´ah mbili na mwishowe aswali Witr kwa Rak´ah moja.

Njia ya nne: Rak´ah kumi na moja. Mtu anaswali nne kwa Tasliym moja kisha afanye hali kadhalika katika zile zengine nne zinazofuata na mwishowe mtu aswali tatu.

Je, alikuwa akikaa baina ya kila Rak´ah mbili wakati anaposwali nne na tatu? Hatukupata jibu lenye kutosheleza katika hilo, lakini haikuwekwa katika Shari´ah pindi mtu anaposwali tatu.

Njia ya tano: Rak´ah kumi na moja. Hapa hakai isipokuwa tu katika ile ya nane na anafanya Tashahhud, anamswalia Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kisha anasimama bila kutoa Tasliym. Halafu anaswali Witr kwa Rak´ah moja kisha anatoa Tasliym. Zinakuwa tisa. Kisha anaswali Rak´ah mbili hali ya kukaa.

Njia ya sita: Aswali Rak´ah tisa na wala asikae isipokuwa katika ile Rak´ah ya sita. Halafu afanye Tashahhud, amswalie Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) n.k.

Hizi ndio namna zilizothibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kuna uwezekano vilevile wa kuongeza namna moja ambayo ni kupunguza idadi ya Rak´ah

mpaka kubaki Rak´ah moja peke yake. Hili ni kujengea maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

> "Yule anayetaka aswali Witr kwa tano, anayetaka aswali Witr kwa tatu na anayetaka aswali Witr kwa moja."[25]

Hizi Rak´ah tano na tatu zinaweza kuswaliwa kwa kukaa mara moja na kutoa Tasliym mara moja kama ilivyo katika njia ya pili. Vilevile yule anayetaka anaweza kutoa Tasliym kila baada ya Rak´ah mbili kama ilivyo katika njia ya tatu, jambo ambalo ndio bora[26].

Ama kuhusu kuswali tano na tatu na kukaa baina ya kila Rak´ah mbili bila ya kutoa Tasliym, ni kitu sikupata kuwa kimethibiti kutoka kwake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Asili ni kuwa inajuzu, lakini Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amekataza kuwitiri kwa Rak´ah tatu na akatoa sababu ya hilo kwa kusema:

> "Isifananishwe na Swalah ya Maghrib."[27]

Kwa hiyo ni wajibu kwa yule anayetaka kuswali Witr Rak´ah tatu aepuke mfanano huu. Hili linakuwa kwa njia mbili:

Ya kwanza: Tasliym kati ya ile isiyokuwa Witr na Witr na hii ndio yenye nguvu na bora zaidi.

Ya pili: Mtu asikae kati ya ile isiyokuwa Witr na Witr na Allaah (Ta´ala) ndiye mjuzi zaidi.

Kisomo katika Witr ambayo ni Rak´ah tatu

[14] Ikiwa Witr ni Rak´ah tatu, basi lililo Sunnah ni kusoma "al-A´laa" katika ile Rak´ah ya kwanza, "al-Kaafiruun" katika Rak´ah ya pili na "al-Ikhlaasw" katika Rak´ah ya tatu ambayo wakati mwingine mtu anaweza kuongeza juu yake "al-Falaq" na "an-Naas".

---

[25] Ameipokea at-Twahaawiy, al-Haakim na wengineo. Hadiyth ina mlolongo wa wapokezi Swahiyh kama walivyosema maimamu wengi. Ina Hadiyth nyingine mfano wake ilio na nyongeza ambayo ni munkari, kama nilivyobainisha katika "Swalaat-ut-Taraawiyh", uk. 99-100

[26] Faida muhimu! Ibn Khuzaymah amesema katika "as-Swahiyh" yake (02/194) baada ya kutaja Hadiyth ya ´Aaishah na nyenginezo juu ya hizo namna zilizotajwa: "Inajuzu kwa mtu kuswali idadi yoyote ya swalah anayotaka katika yale yaliyopokelewa kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)." Haya yanaafikiana na maoni yetu ya kwamba mtu ashikamane na ile idadi iliyosihi kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na mtu asizidishe juu yake. Himdi zote zinamstahikia Allaah kwa mafanikio Yake na ninamuomba ziada katika fadhila Zake.

[27] at-Twahaawiy, ad-Daaraqutwniy na wengineo. Tazama "at-Taraawiyh", uk. 99-100.

Vilevile imesihi kutoka kwake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba alisoma katika Witr Aayah mia moja kutoka katika "an-Nisaa´".

Du´aa za Qunuut na mahala pake

[15] Baada ya kumaliza kisomo na kabla ya kwenda katika Rukuu´, wakati mwingine alikuwa akisoma du´aa ya Qunuut ambayo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alimfunza mjukuu wake al-Hasan bin ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anhumaa):

اللهم اهدني فيمن هديت, وعافني فيمن عافيت, وتولني فيمن توليت, وبارك لي فيما أعطيت, وقني شر ما قضيت, فإنك تقضي ولا يقضى عليك, وإنه لا يذلّ من واليتَ, ولا يعزّ من عاديت, تباركت ربنا وتعاليت، لا منجا منك إلا إليك

> "Ee Allaah! Niongoze pamoja na wale Uliowaongoza, uniafu pamoja na wale Uliowaafu, Uniangalie pamoja na wale Unaowaangalia, Unibariki katika kile Ulichotoa na Unilinde kutokamana na shari kwa yale Uliyohukumu. Kwani hakika Wewe ndiye mwenye kuhukumu na wala Huhukumiwi. Hakika hatwezeki yule Uliyemfanya mpenzi na wala hapati nguvu yule Uliyemfanya adui. Umebarikika na Umetukuka Mola wetu. Hakuna mahali pa kuokoka kutokamana na Wewe isipokuwa Kwako."[28]

Baada ya hapo ni sawa wakati fulani kumswalia Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

[16] Hakuna neno kwa yule atakayesoma Qunuut baada ya Rukuu´ na kama nyongeza akawalaani makafiri, akamswalia Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na akawaombea du´aa waislamu katika ile nusu ya pili ya Ramadhaan. Imethibiti kuwa maimamu kipindi cha ´Umar (Radhiya Allaahu ´anh) walifanya hivo. Imekuja mwishoni mwa Hadiyth ya ´Abdur-Rahmaan bin ´Abd al-Qaariy:

"Walikuwa wakiwalaani makafiri baada ya nusu [ya mwezi]: "Ee Allaah! Wapige vita makafiri ambao wanazuilia na njia Yako, wanawakadhibisha Mitume Wako na wala hawaamini ahadi Yako. Watofautishe, tia woga ndani ya mioyo yao na ufanye utwevu na adhabu Yako viwapate - Ee Mungu wa haki!" Halafu wanamswalia Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wanawaombea kheri waislamu na msamaha waumini. Kisha wanasema: "Ee Allaah! Hakika Wewe ndiye tunakuabudu, Kwako Wewe tu ndiye tunaswali na kusujudu na Kwako ndiko tunakimbilia. Tunataraji huruma Yako, ee Mola

[28] Ameipokea Abu Daawuud, an-Nasaa´iy na wengineo. Mlolongo wa wapokezi ni Swahiyh. Tazama "Swifat-us-Swalaah", uk. 95-96, chapisho la saba.

wetu, na tunakhofu adhabu Yako ya kisawasawa. Hakika adhabu Yako itawapata wale ambao ni adui Zako." Kisha mtu analeta Takbiyr na kusujudu."[29]

Kipi kinachosemwa mwishoni mwa Witr?

[16] Ni Sunnah kusema mwishoni mwa Witr, ni mamoja iwe kabla au baada ya Tasliym:

اللهم إني أعوذ برضاك من سخطك, وبمعافاتك من عقوبتك، وأعوذ بك منك، لا أحصي ثناءً عليك, أنت كما أثنيت على نفسك

"Ee Allaah! Hakika mimi najilinda kwa ridhaa Yako kutokamana na hasira Zako, msamaha Wako kutokamana na adhabu Yako na naomba ulinzi Kwako kutokamana na Wewe. Siwezi kukusifu vile Unavostahiki Wewe ni kama vile Ulivyojisifu Mwenyewe."[30]

[18] Baada ya kumaliza Witr, mtu aseme:

سبحان الملك القدوس, سبحان الملك القدوس, سبحان الملك القدوس

"Ametakasika Mfalme, Mtakatifu. Ametakasika Mfalme, Mtakatifu. Ametakasika Mfalme, Mtakatifu."

Sauti inatakiwa kurefushwa na kuiinua mara ya tatu[31].

Rak´ah mbili zinazofuata

[19] Inafaa kwake kuswali Rak´ah mbili kujengea ya kwamba zimethibiti katika matendo ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)[32]. Bali amewaamrisha nazo Ummah wake na kusema:

[29] Ameipokea Ibn Khuzaymah katika "as-Swahiyh" yake (02/155-156/1100).

[30] Swahiyh Abiy Daawuud (1282) na "al-Irwaa´" (430).

[31] Swahiyh Abiy Daawuud (1284).

[32] Ameipokea Muslim na wengieo. Tazama "al-Irwaa´", uk. 108-109.

"Hakika safari hii ina juhudi na uzito. Baada ya mmoja wenu kuswali Witr, basi na aswali Rak´ah mbili. Ima akaamka au akalipwa kwazo."[33]

[20] Sunnah ni kusoma ndani yake "az-Zalzalah" na "al-Kaafiruun".[34]

I´tikaaf na kuwekwa kwake katika Shari´ah

[1] I´tikaaf ni Sunnah katika Ramadhaan na masiku mengine ya mwaka. Msingi katika hilo ni maneno Yake (Ta´ala):

وَأَنتُمْ عَاكِفُونَ فِي الْمَسَاجِدِ

"Ilihali ni wenye kukaa I'tikaaf misikitini."[35]

Kadhalika kumepokelewa Hadiyth nyingi Swahiyh juu ya I´tikaad yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Vivyo hivyo kumepokelewa mapokezi mengi kutoka kwa Salaf, kama ilivyotajwa katika "al-Muswannaf" ya Ibn Abiy Shaybah na "al-Muswannaf" ya ´Abdur-Razzaaq[36].

Imethibiti ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alifanya I´tikaaf katika yale masiku kumi ya mwisho ya Shawwaal[37] na kwamba ´Umar alisema kumwambia Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

[33] Ameipokea Ibn Khuzaymah katika "as-Swahiyh" yake. Imetajwa katika "as-Swahiyhah". Nilikuwa nimechukua msimamo wa kunyamaza juu ya Rak´ah mbili hizi kwa muda mrefu. Nilipoona amri hii ya kiutume tukufu, nikakimbilia kuitendea kazi na nikatambua maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam): "Ifanyeni swalah yenu ya mwisho iwe ni Witr" ni kwa minajili ya khiyari, na sio malazimisho. Haya ndio maoni ya Ibn Naswr (130).

[34] Ameipokea Ibn Khuzaymah (1104) na (1105) kutoka katika Hadiyth ya ´Aaishah na Anas (Radhiya Allaahu ´anhumaa) kwa sanadi mzili zinazopeana nguvu. Tazama "Swifat-us-Swalaah", uk. 124.

[35] 02:187

[36] Hapa katika lile chapisho lililotangulia kulikuwa Hadiyth juu ya fadhila za kitendo hicho "Yule mwenye kufanya I´tikaaf siku moja... ". Nikaona kuwa ni dhaifu na hivyo nikawa nimeiondosha baada ya kuitaja na kuizungumzia kwa upambanuzi katika "Silsilah al-Ahaadiyth adh-Dhwa´iyfah" (5347). Hapo nimeonyesha kasoro zake zilizokuwa zimefichikana na mimi na kabla yangu al-Haythamiy.

[37] Ni kipande cha Hadiyth ya ´Aaishah iliyopokelewa na al-Bukhaariy na Ibn Khuzaymah katika "as-Swahiyh" zao. Imetajwa katika "Swahiyh Abiy Daawuud" (2127).

"Niliweka nadhiri katika kipindi cha ukafiri ya kwamba nitafanya I´tikaaf usiku mmoja katika msikiti Mtakatifu." Ndipo akasema: "Tekeleza nadhiri yako [na ukae I´tikaaf usiku mmoja]."[38]

[2] Hata hivyo imekokotezwa zaidi katika Ramadhaan. Abu Hurayrah amesema:

"Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akikaa I´tikaaf masiku kumi katika kila Ramadhaan yale ilihali alikaa I´tikaaf masiku ishirini katika ule mwaka alokufa ndani yake."[39]

[3] Lililo bora ni kufanya I´tikaaf mwishoni mwa Ramadhaan, kwa sababu Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akifanya I´tikaaf yale masiku kumi ya mwisho ya Ramadhaan mpaka pale Allaah (´Azza wa Jall) alipomfisha[40].

Sharti zake

[1] Haikuwekwa Shari´ah isipokuwa msikitini tu. Amesema (Ta´ala):

وَلَا تُبَاشِرُوهُنَّ وَأَنتُمْ عَاكِفُونَ فِي الْمَسَاجِدِ

"Na wala msichanganyike nao hali ya kuwa nyinyi ni wenye kukaa I'tikaaf misikitini."[41]

´Aaishah amesema:

"Sunnah kwa yule mwenye kufanya I´tikaaf ni asitoke isipokuwa kwa haja inayomlazimu. Asimtembelee mgonjwa, asimguse mwanamke wake na wala asimwingilie. Akae I´tikaaf katika msikiti unaoswaliwa mkusanyiko. Sunnah pia kwa yule anayefanya I´tikaaf afunge."[42]

[38] Ameipokea al-Bukhaariy, Muslim na Ibn Khuzaymah na nyongeza ni ya al-Bukhaariy katika upokezi mmoja, kama ilivyotajwa katika "al-Mukhtaswar". Imetajwa vilevile katika "as-Swahiyh Abiy Daawuud" (2136-2137).

[39] Ameipokea al-Bukhaariy na Ibn Khuzaymah katika "as-Swahiyh" zao. Imetajwa katika marejeo yaliyotangulia (2126) na (2130).

[40] Ameipokea al-Bukhaariy, Muslim na Ibn Khuzaymah. Imetajwa katika "al-Irwaa´" (966) na "Swahiyh Abiy Daawuud" (2125).

[41] 02:187

[42] Ameipokea al-Bayhaqiy kwa mlolongo wa wapokezi Swahiyh na Abu Daawuud kwa mlolongo wa wapokezi mzuri. Upokezi hapa unaofuata utokamanao kwa ´Aaishah umepokelewa na yeye pia. Imetajwa katika "Swahiyh Abiy Daawuud" (2135) na "al-Irwaa´" (966).

[2] Inatakiwa kufanywa katika msikiti unaoswaliwa swalah ya ijumaa ili mtu asilazimike kutoka msikitini kwa ajili ya kuswali swalah ya ijumaa, kwa sababu kutoka kwa ajili ya kuiendea ni wajibu kwake. ´Aaishah amesema katika Hadiyth iliyotangulia:

"Hakuna I´tikaaf isipokuwa tu katika msikiti unaoswaliwa mkusanyiko."

Baadaye nikaja kupata Hadiyth Swahiyh na inayosema wazi na kukhusisha "misikiti" iliyotajwa katika Aayah kwa ile misikiti mitatu; msikiti Mtakatifu, msikiti wa Mtume na msikiti wa al-Aqswaa. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Hakuna I´tikaaf isipokuwa katika ile misikiti mitatu."[43]

Salaf niliowakuta na maoni haya ni Hudhayfah bin al-Yamaan, Sa´iyd bin al-Musayyib na ´Atwaa´ isipokuwa yeye hakutaja msikiti wa al-Aqswaa. Kuna wengine wamesema ni sawa kwenye misikiti yote ambayo mtu anaswali swalah ya mkusanyiko. Baadhi ya wengine wakaenda kinyume na wakasema ni sawa vilevile hata katika msikiti wa nyumbani kwake. Hapana shaka ya kwamba lililo sahihi zaidi katika suala hili ni kutenda kazi kwa mujibu wa Hadiyth - na Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) ndiye anajua zaidi.

[3] Lililo Sunnah kwa yule anayefanya I´tikaaf afunge, kama ilivyokwishatangulia katika Hadiyth ya ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anhaa)[44]

Ni yepi yanayojuzu wakati wa I´tikaaf?

[1] Inajuzu kwake kutoka kwa ajili ya kutekeleza dharura fulani au kutoa kichwa chake nje ya msikiti ili kioshwe na kichanuliwe. ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anhaa) amesema:

"Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akinitolea kichwa chake wakati anafanya I´tikaaf msikitini na mimi niko chumbani mwangu. Nikamtana [na

[43] Ameipokea at-Twahaawiy, al-Ismaa´iyliy na al-Bayhaqiy kwa mlolongo wa wapokezi Swahiyh kutoka kwa Hudhayfah bin al-Yamaan (Radhiya Allaahu ´anh). Imetajwa katika "as-Swahiyhah" (2786) pamoja na mapokezi yanayoafikiana nayo juu na yote ni Swahiyh.

[44] Ameipokea al-Bayhaqiy kwa mlolongo wa wapokezi Swahiyh na Abu Daawuud kwa mlolongo wa wapokezi mzuri. Imaam Ibn-ul-Qayyim amesema katika "Zaad-ul-Ma´aad": "Haikupokelewa kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuwa alifanya I´tikaaf pasi na kufunga. Bali ´Aaishah amesema: "Hakuna I´tikaaf pasi na swawm." Kadhalika Hakutaja (Subhaanah) I´tikaaf isipokuwa tu pamoja na swawm kama ambavyo vilevile Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakufanya hivo isipokuwa pamoja na swawm. Maoni yaliyo na nguvu katika dalili ni yale waliyomo Salaf, nayo ni kwamba kufunga ni sharti katika I´tikaaf na haya ndio maoni ambayo Shaykh-ul-Islaam bin Taymiyyah alikuwa anaonelea kuwa na nguvu zaidi." Kujengea juu ya hili haikuwekwa katika Shari´ah kwa yule aliyeenda msikitini kwa ajili ya kuswali au kitu kingine akanuia I´tikaaf kwa muda aliyoko huko. Haya ndio yaliyosemwa wazi na Shaykh-ul-Islaam katika "al-Ikhtiyaaraat".

katika upokezi mwingine: nikamuosha nikiwa katika hedhi yangu na hakuna kilichokuwa kikitutenganisha mimi na yeye isipokuwa tu kizingiti cha mlango] na pindi alipokuwa anafanya I´tikaaf alikuwa haingii nyumbani isipokuwa kwa sababu ya dharura fulani."[45]

[2] Inajuzu kwa mwenye kufanya I´tikaaf na mwengineo kutawadha msikitini. Mwanamume aliyekuwa anamfanyia kazi Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alitawadha msikitini wudhuu´ khafifu."[46]

[3] Vilevile inafaa kwake kusimamisha hema dogo nyuma ya msikiti akawa anafanya I´tikaaf ndani yake. ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anhaa) kwa amri ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alimsimamishia Khibaa´[47] pindi (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) anapofanya I´tikaaf[48].

Vilevile kuna wakati alifanya I´tikaaf kwenye kuba dogo ambayo mlango wake ulikuwa umefanywa kwa mkeka.

Inafaa kwa mwanamke kufanya I´tikaaf na kumtembelea mume wake msikitini

[4] Inajuzu kwa mwanamke kumtembelea mume wake wakati anapofanya I´tikaaf kama ambavyo inafaa kwake mwanamume kumuaga kwenye mlango wa msikiti. Swafiyyah (Radhiya Allaahu ´anhaa) amesema:

"Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alifanya I´tikaaf [msikitini katika yale masiku kumi ya mwisho ya Ramadhaan] pindi siku moja nilipomwendea kumtembelea. [Wakeze walikuwa tayari huko lakini wakaenda baada ya muda] na tukazungumza [kwa muda]. Halafu nikasimama ili nende [ndipo akasema: "Usiwe na harak; wacha tufuatane."] Ndipo akasimama ili kunifuata." Makazi yake yalikuwa nyumbani kwa

[45] Ameipokea al-Bukhaariy, Muslim, Ibn Abiy Shaybah na Ahmad na nyongeza ya kwanza ni ya kwao wawili. Imetajwa katika "Swahiyh Abiy Daawuud" (2131-2132).

[46] Ameipokea al-Bayhaqiy kwa mlolongo wa wapokezi mzuri na Ahmad (05/364) kwa ufupi kwa mlolongo wa wapokezi Swahiyh.

[47] Khibaa´ ni kanyumba ka kiarabu kanakotokamana na manyoya au pamba, lakini sio nywele, na kamesimamishwa na nguzo mbili au tatu. (an-Nihaayah)

[48] Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim kutoka kwa ´Aaishah. Kitendo ni cha al-Bukhaariy na amri ni ya Muslim.

Usaamah bin Zayd. [Pindi tulipofika kwenye mlango wa msikiti karibu na mlango wa Umm Salamah] wakapita pambizoni wanaume wawili kutoka katika Answaar. Pindi walipomuona Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), wakaanza kuchapuka. Ndipo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akasema: "Tulieni! Huyu ni Swafiyyah bint Huyayy." Ndipo wakasema: "Ametakasika Allaah! Ee Mtume wa Allaah?" Akasema: "Hakika shaytwaan anatembea kwa mwanaadamu kama inavyotembea damu. Hakika mimi nachelea shari - au kitu - isije kuingia nyoyoni mwenu.""[49]

Inajuzu kwake kufanya I´tikaaf na mume wake au peke yake. ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anhaa) amesema:

"Moja ya wakeze Mtume wa Allaah alifanya I´tikaaf pamoja na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wakati akitokwa na damu ya ugonjwa (na katika upokezi mwingine inasemekana kwamba alikuwa ni Umm Salamah). Alikuwa akiona majimaji mekundu na manjano na hivyo wakati mwingine tulikuwa tunaweza kuweka sahani chini yake na huku anaswali."[50]

Amesema vilevile:

"Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akifanya I´tikaaf yale masiku kumi ya mwisho ya Ramadhaan mpaka pale Allaah (´Azza wa Jall) alipomfisha."[51]

[5] Kitendo hichi kinabatilishwa na jimaa kujengea maneno Yake (Ta´ala):

وَلَا تُبَاشِرُوهُنَّ وَأَنتُمْ عَاكِفُونَ فِي الْمَسَاجِدِ

"Na wala msichanganyike nao hali ya kuwa nyinyi ni wenye kukaa I'tikaaf misikitini."[52]

Ibn ´Abbaas amesema:

"Yule mwenye kufanya I´tikaaf akifanya jimaa, basi I´tikaaf yake inabatilika na anatakiwa kuanza mwanzo."[53]

[49] Ameipokea al-Bukhaariy, Muslim na Abu Daawuud na nyongeza ya mwisho ni ya kwake.

[50] Ameipokea al-Bukhaariy. Imetajwa katika "Swahiyh Abiy Daawuud" (2138). Upokezi mwingine unatoka kwa Sa´iyd bin Mansuur kama ilivyotajwa katika "al-Fath" (04/281). Hata hivyo ad-Daarimiy amesema kuwa anaitwa Zaynab (1/22) - na Allaah ndiye anajua zaidi.

[51] Ameipokea al-Bukhaariy, Muslim na wengineo. Takhriyj yake imeshatangulia kutajwa.

[52] 02:183-187

Hata hivyo halazimiki kutoa kafara kwa sababu haikuthibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Maswahabah wake.

Kutakasika kutokamana na mapungufu na himdi zote ni Zako Allaah. Nashuudia ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Wewe. Ninakuomba msamaha na kutubia Kwako.

Mpaka hapa yanaisha marejeo na masahihisho mapya na zile faida mpya zilizoongezwa na mwandishi. Haya yalikuwa siku ya jumapili tarehe 26 Rajab mwaka 1406 na swalah na salaam zimwendee yule ambaye hakuwa mjuzi wa kuandika wala kusoma Muhammad, familia yake na Maswahabah wake.

´Ammaan, Jordan
Muhammad Naaswir-ud-Diyn al-Albaaniy
Abu ´Abdir-Rahmaan

[53] Ameipokea Ibn Abiy Shaybah (03/92) na ´Abdur-Razzaaq (04/363) kwa mlolongo wa wapokezi Swahiyh.